

MAFUMBO

1. Kaka ufumbapo fumbo, fumba linalofumbika,
Siyo kufumba mafumbo, upesi yakaeleka,
Fumba ulitoe jambo, kwa maneno paka paka,
Ole ulinizunguka, hali nakuangalia.
2. Mimi nilipata tambo, kwa fumbo lisofumbika,
Nikapigwa na kikumbo, na moyo kunilipuka,
Kwani ulisema mambo, ya kunifanya kucheka,
Ole ulinizunguka, hali nakuangalia.
3. Hizi uziimbe nyimbo, bila ya kukasirika,
Ndani yake mna tambo, mawazo ukijitwika,
Ila uache misimbo, na vifumbo kunitwika,
Ole ulinizunguka, hali nakuangalia.
4. Ungelinipiga fimbo, ningelia nikacheka,
Lakini kwa hayo mambo, mbona nimekukiuka,
Leo nisiimbwe nyimbo, kama niliyezuzuka,
Ole ulinizunguka, hali nakuangalia.

Hamidu R. Tambwe
